

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

LEARNING BY EAR 2010
SHALL I TELL YOU SOMETHING?
AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 08: „THE OWL AND THE CICADA“

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAÏMA GUIRA**

TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS

PROOFREADING: TONY DUNHAM

KISUAHELI : ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (male, 40 years old at least)
2. CICADA (female, about 15-20 years old)
3. OLD OWL (female, sounding 60 years old at least)
4. SIMBA THE LION (male, about 30 years old, deep voice)

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

INTRO / PRESENTER:

Hujambo na karibu katika makala ya 8 kwenye msururu wa vipindi vyetu vya Noa Bongo! Jenga Maisha Yako. “Je Nikudokezee” ni hadithi za Kiafrika kuhusu tamaduni na amani. Natumai umejijami vilivyo katika safari yetu kwani leo tunakupeleka hadi katika mlima mmoja wa amani karibu na mto, ambako Bundi na Njenje walikuwa wakiishi. Sikiliza kwa makini ufahamu kwanini wawili hao walizozana katika kutafuta suluhu ya mzozo wao. Sasa basi makinika ili upate uhondo wa hadithi ya “Bundi na Njenje”.

1. MUSIC (*plays in background for the entire script*)

2. SFX : *Sound of a babbling brook*

3. NARRATOR:

Kutoka kilele cha mlima, ungeona mto mfano wa chatu anayegaagaa mchangani. Maji yake yalikuwa safi sana. Kando ya mto huo kulikuwa na miti iliyojipanga kama askari kwenye gwaride la heshima tayari kuwapigia saluti watu wanaotumia madau kwenye mto huo, huku sauti za nyimbo tamu zikisikika kwa mbali.

4. SFX: *River and paddle sounds.*

und wenn möglich: Polyphonic songs??? (Hr. Ndiaye)

5. NARRATOR:

Ni katika eneo hili ambapo Bundi na Njenje walibahatika kuishi kama majirani. Mwanzo walifurahia sana ujirani wao, lakini baada ya

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

muda Bundi alionekana kughadhabishwa na jirani yake mcheshi, ambaye alikuwa na utaratibu wa kuimba kila siku kutoka asubuhi hadi jioni. Siku moja Bundi hakuweza kuvumilia tena na akammua kutoa tetesi zake:

6. SFX: *Chirruping cicada (Archiv: 4016291000)*

7. OWL (kwa hasira):

“Ni nani huyo anayepiga kelele hizo?”

8. CICADA (*kutoka mbali*):

“Ni mimi Njenje mwenye sauti nzuuuuuuuuuuuuri!”

9. OWL:

“Unaweza kuacha kuimba? Sijapata usingizi kwa wiki tatu sasa! Nyimbo zako za kurudiarudia zinanasinya. Na wajua nini....oh, hebu subiri, nitakuja nikueleze peupe!”

10. SFX: *Owls wings flutter*

11. NARRATOR:

Kwa alivyoghadhabika Bundi akaamua kwenda kwa huyo jirani yake ambaye amekuwa akimkera sana.

12. OWL:

“Nilikuwa nasema hivi, kelele zako sasa zimenichosha. Nimevumilia lakini sasa naona umevuka mpaka.”

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

13. CICADA (*perplexed*):

“Hebu subiri kidogo! Kwani nimefanya jambo gani baya bibi Bundi?”

14. OWL:

“Unanikejeli sio? Sikiliza, maisha yangu yote nimekuwa nikiwinda usiku ili kukimu mahitaji ya familia yangu, na wakati wangu wa kupumzika ilikuwa ni huwa mchana tu. Sasa nimestaafu na kuamua kuishi katika eneo hili la mashambani lenye amani ili nipumzike na kufurahia siku zangu za mwisho kabla sijafa. Sioni ni kwa sababu gani mtoto kama wewe utakuja kunihangaisha hapa. Na nikisema hivyo, sina ubaya na wewe, lakini hebu nieleze tafadhali ni nini kinachokufanya uimbe usiku kucha?”

15. CICADA:

“Bibi, lazima ujue kwamba mimi ni mcha Mungu sana, na kuimba hizi nyimbo zangu ni namna moja ya kumsifu Mola wangu. Na kwa taarifa, yako hizo nyimbo ujue zinaitwa ‘zikr’.”

16. OWL:

“Sikujua kwamba ulikuwa unafanya ibada, lakini sawa, hebu tuzungumzie hiyo dini yako. Si nguzo mbili muhimu katika kila dini ni uvumilivu na heshima kwa jirani yako? Sasa pengine ingekuwa bora

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

kama ungenifikiria mimi pia! Na kama wewe ni mcha Mungu kweli kama unavyodai, kwanini usijenge hekalu lako katika sehemu nyingine, ili uwe mhubiri na wafuasi wako waweze kufuata dini yako vizuri? Pia unaweza kuwa shirika na vunja jungu ambaye bila shaka atafurahi sana kuwa mfuasi wako. Bila shaka, mtakuwa na muingiliano.”

17. CICADA :

“Sitabishana na wewe bibi, kama ningeweza tu kukueleza...”

18. OWL:

“Sikiliza binti yangu, nishasema ya kutosha! Hivi unavyoniona nimechoka na pia nasinzia kweli. Wewe njoo unione baada ya kuuyatafakari masharti niliyokupa ili tuzungumze kwa lengo la kujenga uhusiano zaidi na kuishi kwa amani.”

19. NARRATOR:

Alipojiona yuko peke yake, Njenje akaanza kutafakari maoni ya jirani yake. Na kadri siku zilivyosonga alizidi kukereka na kunung'unika!

20. CICADA (to herself):

“Mimi siwezi kuishi bila ya kuimba. Ni jambo ninalolipenda sana, ndio sasabu ya kuishi kwangu hapa duniani. Nitakuwa nimepata hasara kubwa kuacha kuimba kwa sababu tu ya kumridhisha yule ndege aliyezeeka! Ahhh ...Amezidi mno!”

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

21. SFX: *CICADA STARTS SINGING (Archiv: 4016291000)*

22. NARRATOR:

Na sasa Njenje akaanza kuimba kwa nguvu zaidi. Hata hivyo, wakati mwingine alikuwa akijilaumu sana alipofikiria maneno ya Bundi.

23. CICADA (*to herself*):

“Nadhani haipendezi kwa mtu kuendelea kusumbuliwa kama ametimia umri kama huu wangu. Kwa kweli pengine ningeacha kuimba. Lakini nikiacha kuimba nitafanya nini? Ujenzi? Nitumie muda wangu wote kujenga nyumba, viota na makaburi? La hashu! Haiwezekani japo hali hii inanitatiza.”

24. NARRATOR:

Na hapo Njenje alikuwa amechanganyikiwa sana hadi akaamua kwenda kumtembelea Bundi tena:

25. SFX: *Chirruping cicada (Archiv: 4016291000)*

26. CICADA:

“Ni mimi tena Bibi. Nimekuja kukueleza, sitaki unikasirikie namna hiyo mpaka inafika kiwango kwamba hatuwezi kusemezana tena.”

27. OWL:

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

“Sidhani kwamba naweza kuzungumza nawe tena Njenje!
Unayosema hata hayamo akilini mwangu. Hata hivyo naweza tu
kuzungumza nawe tena endapo utaacha kuwa na ubinafsi kujifikiria
wewe tu. Kwa hivyo wacha hilo liwe funzo kwako. Kwa sasa niache
nipumzike, njoo unione wakati mwingine.”

28. NARRATOR:

Ilimbidi Njenje aondoke huku akiwa amevunjika moyo kutokana na
jinsi Bundi alivyomchukulia.

29. CICADA:

“Hawa wazee hawaelewi kwamba dunia imebadilika! Yaani wao
wakishafanya maamuzi hawataki kupingwa!”

30. NARRATOR:

...Njenje alihema kwa nguvu na alipokuwa nyumbani ghafla
akashikwa na homa kutokana na ghadhabu. Kuimba kwake kukawa
nadra sana. Wakati mwingine aliimba lakini wakati mwingine
alinyamaza kimya siku nzima. Tabia yake ngeni pia ikamshtua
Simba, mfalme wa Savana. Simba aligundua tabia hii mara ya
kwanza alipokuwa katika ziara yake katika nchi hiyo kukutana na
wanyama wengine. Lakini akamkuta Njenje akiwa hana furaha na
hata kukataa kujibu salamu zake. Jambo lililomkasirisha Mfalme
Simba.

31. SIMBA THE LION roars

32. SIMBA THE LION:

“Njenje mbona una huzuni namna hiyo? Kwani umepatwa na

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

msiba? Kawaida tunasikia nyimbo zako hata kabla ya kukuona, lakini siku hizi hatukusikii tena kabisa.”

33. NARRATOR:

Njenje akamuelezea Simba masaibu yake yote. Na baada ya kusikiliiza kwa makini, Simba akarudi hadi katika kasri yake na kuitisha mkutano wa dharura na kamati kuu ya wazee, akiwemo Ndovu, Kobe, Beberu pamoja na Kinyonga. Kisha wakawaita Njenje na Bundi. Baada ya mazungumzo yaliyopamba moto, Mflame Simba akatoa uamuzi kwa sauti yake nzito:

34. SIMBA THE LION:

“Tumefikiria kwa makini kuhusu mzozo huu wenu na haikuwa rahisi kufikia maamuzi tutakao utoa. Wewe Njenje umeonyesha heshima yako kwa mtu mzima! Ulikuwa tayari kuacha kuimba ili kumridhisha Bundi. Na wewe Bundi, kwa heshima yote tunayokupa, nadhani ni vyema ungepuuza tabia ya Njenje ya kuimba. Huyu Njenje ni ndege mdogo ambaye anaendelea kukua, na tunajua kwamba wakati mwingine kuimba kwake kunaweza kukera. Hata hivyo lakini, tunampenda. Sasa basi tungependa ninyi wawili mtilie maanani kwamba, hatua ya kwanza katika kutataua matatizo ni kukubaliana na kuheshimiana.”

35. NARRATOR:

Kufikia hapo, mkutano ukavunjwa na kila mmoja akarejea nyumbani kwake. Busara ya Simba zikamridhisha kila moja. Njenje akarejelea utaratibu wake wa kuimba bila pingamizi yoyote lakini safari hii

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

akiwa mwangalifu zaidi kuliko awali. Na wakati Bundi alipohitaji kupata usingizi aliruka tu juu ya mti kidogo ambako hangeweza kusikia nyimbo za Njenje...

36. SFX : *Chirruping cicada (Archiv: 4016291000)*

37. NARRATOR:

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu..

38. Music

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 08 The owl and the cicada

Author: Ibrahima Ndiaye

OUTRO:

Kwa mara nyingine hadithi yetu inaonyesha kwamba kuna mbinu za kutatua mizozo zinazoweza kumridhisha kila mtu. Japokuwa Bundi alionekana kutomuelewa Njenje kwa namna mmoja au nyingine, ilimbidi waishi pamoja kwa amani. Je wewe? Unaweza kujinyima kwa ajili ya kumridhisha mwenzako? Na je, unaonyesha vipi heshima yako kwa watu wazima? Waulize rafiki zako, na jadiliana na bibi au babu yako kisha utufahamisha kwa kutumia anuani ifuatayo lbe@dw-world.de.

Usikose kujiunga nasi tena kujifunza mengi kupitia vipindi vyetu vya Noa Bongo! Jenga Maisha Yako. Na iwapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vingine vinavyotayarishwa na Deutsche Welle tembelea mtandao wetu: www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwingine, kwaheri kwa sasa!

END